JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

Simu Na. 023 2935403
Nakishi. 023 2935402

**Barua pepe**
ded@chalinzedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 65,
**CHALINZE**

16/11/2021

**Kumb. Na.** HWC/CMT/2021/10

Mwenyekiti na Wajumbe,
Kamati ya Wataalam (CMT),

**YAH: MWALIKO WA KUHUDHURIA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAM (CMT) CHA KUPITIA TAARIFA ZA MWEZI OKTOBA 2021**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Unaalikwa kuhudhuria kikao cha kamati ya wataalam (CMT) cha kupitia taarifa za mwezi Oktoba 2021 kitakachofanyika tarehe 18/11/2021 siku ya Alhamisi katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Chalinze kuanzia saa 3:00 Asubuhi.

Hivyo, kwa barua hii unakaribishwa kuhudhuria kikao hicho bila kukosa

Ahsante

GEOFREY MWALUKASA
**K/AFISA UTUMISHI NA UTAWALA WILAYA**
**CHALINZE**

## AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAM (CMT) MWEZI OKTOBA 2021

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUTHIBITISHA AGENDA
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 13/10/2021
4. YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 13/10/2021
5. KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA FEDHA – MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI OKTOBA, 2021
6. TAARIFA YA UTUMISHI NA UTAWALA YA MWEZI OKTOBA, 2021
7. TAARIFA YA UTENDAJI KAZI KITENGO CHA TASAF
8. TAARIFA YA HALI YA MAREJESHO KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA 2021.
9. TAARIFA YA MIZINGA YA NYUKI KUTOLEWA KWA NJIA YA MKOPO BADALA YA RUZUKU.
10. KUPITIA MUHTASARI WA KAMATI YA FEDHA WA MWEZI SEPTEMBA 2021 NA YATOKANAYO YAKE.
11. MENGINEYO
12. KUFUNGA KIKAO

# AGENDA Na. 3

## KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 13/10/2021

(UKURASA WA 01 – 21)

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

## MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI KILICHOJADILI TAARIFA ZA ROBO YA KWANZA JULAI-SEPTEMBA 2021/2022 KILICHOFANYIKA TAREHE 13/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MASAFA

**MAHUDHURIO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bw.Ramadhani S. Possi | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Mwenyekiti |
| 2. Bi.Jane S. Mfuko | Afisa Utumishi na Utawala(W) | Katibu |
| 3. Bw. Thomas Mollel | K/Katibu Tawala Wilaya(B) | Mjumbe |
| 4. Bw.Shabani K. Millao | Afisa Mipango na Ufuatiliaji(W) | Mjumbe |
| 5. Bi. Anne Mwandiga | Afisa Manunuzi (W) | Mjumbe |
| 6. CPA(T).Said H.Khalid | K/Mweka Hazina(W) | Mjumbe |
| 7. Bw. Paulo Mzumbwe | K/Mhandisi Ujenzi(W) | Mjumbe |
| 8. Bibi Salama Ndyetabura | Afisa Elimu Sekondari(W) | Mjumbe |
| 9. Bw. Reginald Lyimo | Afisa Nyuki(W) | Mjumbe |
| 10. Bw. Musa Kichumu | K/Afisa Ardhi na Maliasili | Mjumbe |
| 11. Bw.Michael H. Maganga | Mkaguzi wa Ndani (W) | Mjumbe |
| 12. Bw.Jonathan P. Shenyagwa | Afisa Usafirishaji(W) | Mjumbe |
| 13. Bw. Rasmo Msabaha | K/Mganga Mkuu(W) | Mjumbe |
| 14. Bi.Miriam S, Kihiyo | K/Afisa Elimu Msingi(W) | Mjumbe |
| 15. Bw.Michael Mwakanjuki | Mratibu wa TASAF (W) | Mjumbe |
| 16. Bw.Seth Mgonja | K/Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika(W) | Mjumbe |
| 17. Wakili Rosemary S. Kamugisha | Mwanasheria (W) | Mjumbe |
| 18. Bw.Msongo Songoro | Afisa Mifugo | Mjumbe |
| 19. Bw.Yadunia K.Iddi | K/Afisa TEHAMA | Mjumbe |
| 20. Bw.Balthazary Mitti | TEO-CHALINZE | Mjumbe |
| 21. Bi.Zuraika Kundya | Afisa Usafi na Mazingira(W) | Mjumbe |
| 22. Bi.Wahda Mwishehe | K/Afisa maendeleo ya jamii(W) | Mjumbe |

**SEKERITARIETI**

| | |
|---|---|
| 1.Bw .Rodrick R. Kagaruki | Mwandishi wa vikao |
| 2. Bw.Paulo Gwimile | Mwandishi wa vikao |
| 3. Bi.Huluda Malangalila | Mwandishi wa vikao |

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.01/2021-2022 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe na kueleza kuwa kikao hiki ni cha kawaida cha kujadili taarifa za Idara za robo ya kwanza Julai-Septemba aidha kabla ya kumkaribisha mwenyekiti kufungua kikao Katibu alitoa utambulisho wa Mkaguzi wa Ndani aliyehamia Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na Pia, Bw. Thomas Mollel ambaye alimwakilisha Katibu Tawala wa Wilaya ya Bagamoyo baada ya utambulisho huo alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufungua kikao ambapo alifungua saa 03:58 Asubuhi.

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.02/2021-2022 KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilithibitishwa na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 17/09/2021
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 17/09/2021
5. Kupokea na kujadili Taarifa ya Fedha – Mapato na Matumizi kwa mwezi Septemba 2021
6. Kupokea na kujadili taarifa ya Idara ya Utumishi na Utawala mwezi Septemba 2021
7. Taarifa ya Mkaguzi wa ndani kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai-Septemba 2021/2021
8. Taarifa ya Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022 ( Julai- Septemba 2021)
9. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Idara kwa Kipindi Cha robo ya kwanza 2021/2022 ( Julai- Septemba 2021)
    I. Taarifa ya utekelezaji Kitengo cha Sheria
    II. Taarifa ya utekelezaji Kitengo cha Manunuzi
    III. Taarifa ya utekelezaji Kitengo cha TEHAMA na mawasiliano
    IV. Taarifa ya Utekelezaji Idara ya Maendeleo ya Jamii
    V. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Elimu Msingi
    VI. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Elimu Sekondari
    VII. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Afya
    VIII. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
    IX. Taarifa ya utekelezaji Kitengo cha nyuki
    X. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Ardhi na Maliasili
    XI. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Usafi na Mazingira
    XII. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Ujenzi
    XIII. Taarifa ya utekelezaji Idara ya Mifugo na Uvuvi

10. Kupitia mihtasari na yatokanayo na vikao vya kamati za kudumu vya robo ya nne 2020/2021
    (i)Kamati ya Fedha Uongozi na Mipango
    (ii)Kamati ya Elimu Afya na Maji
    (iii)Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
11. Taarifa Mbalimbali
12. Kufunga Kikao

**HWC/CMT/MUH NA.03/AG.03/2021-2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 17/09/2021**

Muhtasari wa kikao cha tarehe **17/09/2021** ulisomwa na kufanyiwa marekebisho yafuatayo ukurasa **19** kusomeka kusudio la kuvunja mkataba na si Taarifa ya kuvunja

mkataba.Baada ya marekebisho hayo muhtasari ulithibitishwa na kusainiwa kuwa kumbukumbu sahihi.

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.04/2021-2022 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 17/09/2021**

Yatokanayo na kikao cha tarehe **17/09/2021** yalisomwa na utekelezaji wake kama ifuatavyo;-

**AZIMIO NA. 01**

Wadaiwa (defaulters) wote wapya na wa zamani kuandikiwa barua za kulipa madeni yao ndani ya siku 7

**UTEKELEZAJI**

Yaliwasilishwa majibu ya utekelezaji kuwa, wadaiwa wote wameandikiwa barua ya kuwataka walipe madeni yao ndani ya siku 7

Wajumbe walipokea taarifa na baada ya kupokea taarifa hiyo Mwenyekiti alishauri kuwa kama wamepewa barua na hawajarejesha na wala hawajajibu chochote wachukuliwe hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kuwasimamisha kazi. Aidha, ilielezwa kuwa kwa mmoja ambaye ameanza kurejesha asisitizwe aendelee kurejesha.

***AZIMIO***

*Mwenyekiti aliagiza wadaiwa wote wa defaulters kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kuandikiwa barua za kusimamishwa kazi.*

**AZIMIO NA.02**

Kufanya ufuatiliaji kwenye makampuni yanayojishughulisha na uchimbaji madini kujiridhisaha kama wana cheti kutoka EPZA na kama bado zinafanya kazi.

**UTEKELEZAJI**

Yaliwasilishwa majibu ya utekelezaji kuwa, Ufuatiliaji umefanyika kwenye makampuni ya madini na viwanda na kwenye ukaguzi huo ni kiwanda cha H&J ndiyo chenye cheti cha EPZA. Aidha, ilielezwa kuwa mrabaha ni makubaliano kati ya Halmashauri na Mwekezaji.

Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji na kushauri yafuatayo:-

**USHAURI**

i. Mwenyekiti alishauri ufuatiliaji uendelee kwa upande wa ushuru wa mrabaha
ii. Makampuni yote yafuatiliwe pamoja na kuweka kikao maalum na Mkurugenzi
iii. Mwanasheria aliweke suala hili la ushuru wa mrabaha kwenye sheria ndogo za Halmashauri.

**AZIMIO NA.03**

Kuweka takwimu za kiasi cha fedha kinachotakiwa kufanyiwa mabadiliko na mchanganuo wa gharama za vifaatiba vinavyohitajika kununuliwa kwa Zahanati zote 11 zinazotakiwa kufunguliwa

**UTEKELEZAJI**

Yaliwasilishwa majibu ya utekelezaji kuwa, Fedha zinazofanyiwa mabadiliko ni **Tshs 400,000,000** toka kwenye kituo cha Afya Msata na kupelekwa kwenye ununuzi wa Vifaa tiba kwa Zahanati 11 zilizokamilika.

Wajumbe walipokea taarifa ya utekelezaji na kuhoji yafuatayo:-

**Hoja Na. 1**

Kwanini kiasi cha fedha cha gharama za vifaa tiba ni pungufu ya kiasi husika kilichotengwa?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, kwa mujibu wa takwimu na gharama zilizowekwa na vifaa tiba ni sahihi kwa majibu ya Mganga Mkuu.

**USHAURI**

i. Vinunuliwe viti kwanza badala ya vifaa tiba
ii. Zichaguliwe Zahanati za kuanza nazo ili kuhakikisha zitakazochaguliwa zinakamilika na kuanza kufanya kazi.
iii. Ofisi ya Mipango na Mganga Mkuu waweke mchanganuo unaoeleweka ukionesha gharama za viti na vifaa tiba kwa kila kituo.

***AZIMIO***

*Kuweka takwimu za kiasi cha fedha kinachotakiwa kufanyiwa mabadiliko na mchanganuo wa gharama za vifaa tiba vinavyohitajika kununuliwa kwa zahanati zote **11** zinazotakiwa kufunguliwa.*

**AZIMIO NA.04**

Mweka Hazina kupanga ratiba ya kutembelea vyanzo vya mapato ili kubaini changamoto kwa kila chanzo.

UTEKELEZAJI

Yaliwasilishwa majibu ya utekelezaji kuwa, ratiba ya kutembelea vyanzo vya mapato itaanza kutekelezwa Mwezi Oktoba 2021

Wajumbe hawakuridhika na majibu yaliyowasilishwa na kuhoji yafuatayo:-

**Hoja Na. 1**

Kama ni mwezi Oktoba kwanini ratiba bado haijapangwa wakati mwezi wenyewe ndiyo huu?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, kuanzia wiki lijalo ratiba itapangwa na wakuu wa Idara wataenda kutembelea vyanzo vya mapato.

Mwenyekiti aliagiza ratiba ipangwe iwasilishwe kwenye kikao kabla hakijafungwa

***AZIMIO***

*Kuletwa kwa ratiba ya wakuu wa idara na vitengo kutembelea vyanzo vya mapato siku ya tarehe 13/10/2021.*

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.05/2021-2022 TAARIFA YA FEDHA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI SEPTEMBA 2021**

Wajumbe waliwasilishiwa taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Septemba 2021 kama ifuatavyo;

(A)MAPATO

Taarifa ilieleza kuwa Halmashauri ya Chalinze ilipanga kukusanya kiasi cha fedha **Tshs 50,149,389,520.00** katika bajeti ya mwaka **2021/2022** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwa **Tsh 10,758,818,162.00** ni makisio ya mapato ya ndani na **Tshs 896,568,180.17** ikiwa ni lengo la kukusanya mapato ya ndani kwa mwezi.

Kwa mwezi Septemba, **2021**, Halmashauri ilikusanya Jumla ya **Tshs 3,449,449,644.91** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama ilivyo kwenye takwimu za hapa chini ambayo ni sawa na **21.62%** kwa lengo la mwaka kwa na asilimia **112.70%** kwa lengo la mwezi kwa mapato ya ndani. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Mapato ya ndani | Tshs | 669,360,194.12 |
| Huduma za Afya | Tshs | 19,853,291.75 |
| Ada za shule | Tshs | 38,595,720.00 |
| Michango ya Jamii | Tshs | 282,586,161.90 |
| **Jumla ndogo mapato ya ndani** | **Tshs** | **1,010,395,367.77** |
| Mishahara (Ruzuku) | Tshs | 1,812,710,550.00 |
| Mapato Mengineyo (Ruzuku) | Tshs | 58,824,818.44 |
| Miradi ya maendeleo Ruzuku | Tshs | 567,518,908.70 |
| **Jumla ndogo Ruzuku** | **Tshs** | **2,439,054,277.14** |
| **JUMLA KUU** | **Tshs** | **3, 449, 449,644.91** |

**(B) MATUMIZI**

Taarifa ilieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ilipanga kutumia **Tshs 50,149,389,520.00/=** katika bajeti ya mwaka **2021/2022**, hivyo kwa mwezi Septemba 2021 Halmashauri ilitumia kiasi cha **Tshs 2,779,435,941.70/=** kama takwimu zinavyoonesha hapa chini:-

| | | |
|---|---|---|
| Mapato ya ndani (matumizi kawaida) | Tshs | 237,559,009.00 |
| Mapato ya ndani(miradi) | Tshs | 417,063,274.00 |
| Huduma za Afya | Tshs | - |
| Ada za shule | Tsh | - |
| Michango ya jamii | Tsh | - |
| **Jumla ndogo Matumizi (Mapato ya Ndani)** | **Tshs** | **654,622,283.00** |
| Mishahara (Ruzuku) | Tshs | 1,812,710,550.00 |
| Matumzi Mengineyo (Ruzuku) | Tshs | 37,564,700.00 |
| Miradi ya maendeleo Ruzuku | Tshs | 274,538,408.70 |
| **Jumla ndogo Ruzuku** | **Tshs** | **2,124,813,658.70** |
| **JUMLA KUU** | **Tshs** | **2,779,435,941.70** |

Wajumbe walipokea taarifa. Aidha, Mwenyekiti baada ya kupokea taarifa hiyo alisisitiza juhudi za ukusanyaji wa mapato hasa kwenye mapato ya ndani (proper) na kuhoji yafuatayo:-

**Hoja Na. 01**

Ni mikakati ipi ya Idara imewekwa katika kuhakikisha mapato yanapanda?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, tayari idara imeweka mikakati mipya ikiwemo mabadiliko ya task force katika kuhakikisha kuna ufanisi wa ukusanyaji mapato.

**Hoja Na. 02**

Kwanini ushuru wa vibali vya sherehe na ngoma upo chini wakati sherehe na ngoma zinafanyika kila siku.

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, mapato ya ushuru huu huwa unakusanywa Zaidi hasa kipindi cha ngoma mwezi Disemba.

Mwenyekiti aliagiza ufuatiliaji ufanyike kwa kina. Aidha, alishauri taarifa hiyo iwasilishwe siku ya jumatatu ya tarehe 18/10/2021

**Hoja Na. 3**

Je, chanzo hiki kinakusanywa kwenye vijiji au Halmashauri?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, Halmashauri inakusanya na vijiji pia vinakusanya. Aidha, ilielezwa kuwa sherehe hizi ni za msimu na mara nyingi zinafanyika kuanzia Mwezi Novemba na Mwezi Desemba.

**USHAURI**

Taarifa ya vibali vya sherehe iwasilishwe kila wiki

**Hoja Na. 4**

Kwanini ushuru wa leseni za vileo na Biashara upo chini?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, ufuatiliaji unaendelea na kikao kijacho kutakuwa na mabadiliko.

**Kuhusu chanzo cha mapato cha Redio**

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa taarifa imeletwa kuwa ndani ya mwezo Oktoba 2021 frequency itakuwa tayari na redio itaanza kufanya kazi.

**Hoja Na. 5**

Kwanini ushuru wa mpunga kwa mwezi Septemba 2021 haujakusanywa?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, kwa mwezi Septemba 2021 fedha zimekusanywa zipo kwenye POS.

**Hoja**

Je, lengo litafikiwa kwa kiasi kinachokusanywa?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, ufuatiliaji na usimamizi utawekwa kuhakikisha mapato yanaongezeka.

Mjumbe alieleza kuwa biashara ya Mpunga haipo lakini kuna biashara ya mchele
Mtaalam alilipokea na kukiri kuwa ni kweli biashara inayofanyika ni ya mchele

**USHAURI**

Ufuatiliaji ufanyike zaidi katika chanzo hiki ili kuongeza makusanyo.

**Kuhusu ushuru wa Matunda**

Mjumbe alisema kwa upande wa mananasi alisema ni msimu mmoja tu na zaidi yapo mwezi Desemba ndiyo maana kwa miezi mingine ushuru wa matunda unakuwa mdogo ni kutokana na uzalishaji.

Kuhusu ushuru wa mihogo kuwa chini
Mwenyekiti alishauri ufuatiliaji ufanyike kwenye chanzo hiki

USHAURI

1. Mwenyekiti alishauri Afisa Utamaduni kuwasiliana kwa ukaribu na watendaji wa Kata na Vijiji ili apate ushirikiano kutoka kwao kuweza kukusanya mapato haya kwa ufanisi zaidi kwani sherehe hizi na ngoma zinafanyika kila siku lakini mapato yake ni madogo.
2. Kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa leseni ya vileo
3. Afisa kilimo kuhakikisha tunapoelekea kipindi cha mavuno kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana mazao kama Mpunga,mihogo na mananasi

**Hoja Na. 06**

Kwanini ushuru wa uuzaji mifugo kutoka kwenye minada umeshuka?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, changamoto ipo kwa kipindi hiki ambapo mifugo mingi ipo kwenye malisho haipelekwi mnadani

USHAURI

i. Ufuatiliaji ufanyike zaidi kwenye mnada wa Ruvu darajani
ii. Ifanyike doria kwenye eneo la mapakulio ya Mifugo Ruvudarajani

**Kuhusu ushuru wa Samaki**

Ufuatiliaji unaendelea ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wachuuzi.

Kuhusu paking ya malori wajumbe walihoji yafuatayo:-

**Hoja**

Kwanini chanzo kimewekwa wakati hakipo na hakijaanza kufanya kazi?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, itafanyika review mwezi Desemba kwa vyanzo ambavyo vimewekwa lakini bado havipo vizuri

**Kuhusu mauzo ya viwanja** wajumbe walihoji yafuatayo:-

**Hoja**

Kwanini viwanja haviuzwi?

**Jibu Na. 1**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, linasubiriwa tangazo ambapo dokezo lilishapelekwa kwa Mweka Hazina muda mrefu.

Mwenyekiti alishauri mweka Hazina atoe vipaumbele kwenye vitu muhimu ambavyo vitaiingizia mapato Halmashauri.

**USHAURI**

Suala la uuzwaji wa viwanja Msolwa lipewe kipaumbele.

**Hoja Na. 2**

Ni hatua gani zilizofikiwa kwenye zoezi la upimaji wa eneo la msolwa kwa ajili ya mradi viwanja.

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, vitu vingi vimeshafanyika hatua inayofuata ni kufanya uthamini.

Mwenyekiti alishauri kuwa kazi zifanyike bila kujali uwezeshwaji. Aidha, alishauri kusaidiana katika utekelezaji wa majukumu bila kujali kipato.

Kuhusu NHIF kutoingiziwa fedha kwa miezi mitatu

Wajumbe walishauri Ufuatiliaji ufanyike mapato ya NHIF yaingizwe kwa miezi yote mitatu

Kuhusu ushuru wa Mabanda ya Chakula

Wajumbe waliagiza ufuatiliaji kwenye ukaguzi wa mabanda ya chakula ufanyike ili kuhakikisha mapato yanapatikana.

**Matumizi (kuchaji kifungu husika)**

Ilielezwa kuwa ufuatiliaji umeanza baadhi ya wakuu wa Idara wameanza kuzingatia kwa kuandika vifungu kwenye dokezo

**USHAURI**

i. Ziandaliwe fomu maalum kwa wakuu wa Idara

ii. Mwenyekiti alishauri Fedha zinapoingia taarifa itolewe kwenye kikao

Mweka Hazina alipokea ushauri wa Mwenyekiti na kuahidi kuufanyia kazi japo alisema bado kuna changamoto kwa upande wa matumizi

Wajumbe walipokea maelekezo na kuhoji yafuatayo:-

**Hoja**

Inawezekanaje kuna changamoto ya matumizi?

**Jibu**

Yaliwasilishwa majibu kuwa, ushauri utafanyiwa kazi kila Idara itapewa kidogokidogo.

Aidha, mjumbe alisema fedha za Mitihani bado hazijalipwa

Mwenyekiti aliagiza Mweka hazina alifanyie kazi fedha zitoke kazi ziendelee. Aidha, alisema Ofisi ya Fedha ifanye kazi zake vizuri pamoja na kukusanya mapato ipasavyo. Pia alisema fedha zitolewe kwa vipaumbele.

USHAURI

i. Mweka Hazina akae vikao na watumishi wake
ii. Mkurugenzi amsaidie Mweka Hazina kutokana na kuzidiwa na madeni ya watu.
iii. Madai ya kisheria yalipwe yabaki madeni ambayo hayapo kisheria.
iv. Suppliers wote wawekwe kwenye pool wahudumie kwa usawa.
   Mwenyekiti alipokea ushauri wa Wajumbe.
v. Pamoja na mambo yote Mweka hazina ajipange asimame kwenye 40% za miradi ya Maendeleo.
vi. Stahiki za wakuu wa Idara zilipwe kwa kupunguza punguza mmoja mmoja badala ya kulipa kwa ujumla fedha zinakuwa nyingi uwezo wa kulipa zote kwa pamoja unakuwa mdogo. Pia, wajumbe walishauri uwekwe utaratibu mzuri wa kulipa stahiki kwa wakuu wa Idara.
vii. Mweka hazina aweke utaratibu kwenye fedha za recurrency kwamba kipi kinalipwa kwenye recurrency.
viii. Ikiwezekana stahiki za Wakuu wa Idara zilipwe hadi siku za mbele.
   Wajumbe walikubaliana kwa fedha ambazo tayari zilikuwa zipo kwenye mchakato zilipwe ndipo mfumo mwingine utumike kwa siku za baadaye wa kulipa miezi sita.

Hoja Na.07

Mwenyekiti alihoji kuhusu ushuru wa uuzaji wa fomu za viwanja na gharama za upimaji.

**Hoja Na.05**

Mwenyekiti alihoji kuhusu hatua zilizofikiwa kwenye zoezi la upimaji wa eneo la msolwa kwa ajili ya mradi viwanja.

**Jibu**

Mjumbe alieleza kuwa kazi ilisimama kidogo kutokana na changamoto ya uwezeshaji malipo kwa vijana walipo site kwa ajili ya kazi hiyo.

Mwenyekiti alieleza hatuwezi kusimamisha kazi kwa ajili ya malipo ya posho mradi huu ni mkubwa utakaoenda kuingizia Halmashauri mapato makubwa ni vyema kazi ikandelea na pindi fedha zitapopatika hao watumishi watalipwa posho zao.

AZIMIO

Zoezi la upimaji viwanja eneo la msolwa liendee na kikao kijacho mrejesho uletwe kwenye kikao mradi upo hatua gani.

**Jibu**

Mjumbe alieleza kuwa kiasi cha **Tsh 1,478,000** kilikuwa kimekusanywa kutoka kwenye vyanzo hivyo.

Hoja Na.06

Mwenyekiti alihoji kuhusu madai yetu Bima ya Afya Zaidi ya **Tsh 228,233,000** tangu mwezi Julai-Septemba 2021 hawajarejesha shida ni nini.

**Jibu**

Mjumbe alieleza kuwa tayari madai yaliwasilishwa ofisi za Bima ya Afya mkoani Kibaha lakini lakini fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa.

AZIMIO

Kufanya ufuatiliaji wa madai ya Halmashauri ya Zaidi **Tsh 228,233,000** katika Bima ya Afya na kuleta Mrejesho kikao kijacho

**USHAURI WA JUMLA**

i. Mweka Hazina kuhakikisha anaenda Field na kutembelea vyanzo vyote vya mapato kuhakikisha hakuna ufujaji wa mapato.
ii. Fedha zinapoletwa za Ruzuku OC Taarifa itolewe kwa Menejimenti.
iii. Mweka Hazina kulipa kwa kuzingatia asilimia 60%-40%.

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.06/2020-2021 TAARIFA YA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA MWEZI JULAI- SEPTEMBA 2021/2022**

Taarifa ya Utumishi na Utawala iliwasilishwa na Idara husika. Taarifa hiyo kwa muhtasari ilieleza shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022 (Julai-Septemba 2021) ikiwa ni pamoja na:-

i. Kushughulikia na kutekeleza maagizo mbalimbali na kuhudumia wateja wa ndani na nje.
ii. Kuandaa na kuingiza taarifa zinazohusu bajeti ya Mishahara (PE) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo taarifa zilihusu watumishi kupanda vyeo, kubadilishiwa miundo ya Utumishi, Kutenga nafasi za ajira mpya na kutenga bajati kwa nafasi za uteuzi kwa wakuu wa Idara na Vitengo ambavyo vinakaimiwa.
iii. Kuendelea na zoezi la kuhakiki taarifa za watumishi na sifa za kimuundo kupitia Mfumo wa Mishahara wa watumishi (HCMIS)
iv. Kusimamia uwajibikaji na Nidhamu ya Watumishi.
v. Kushughulikia stahiki mbalimbali za waheshimiwa Madiwani na Watumishi.
vi. Kuratibu watumishi wanaohama, kuhamia, Kufariki na kustaafu Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ambapo watumishi **22** wamehamia chalinze maeneo mengine ya kazi wakiwemo walimu 17, mchumi 01 na afya mtumishi 01,Afisa kilimo Msaidizi 01,Muuguzi 01,Mhudumu wa Afya 01. watumishi waliohama jumla **28**,walimu 22 Afya 03,Mtendaji kijiji 01,Dereva 01,Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa ndani 01 watumishi waliofariki katika kipindi cha mwezi Julai-Septemba 2021 ni **03**. Waliostaafu kwa kipindi cha Julai-Septemba 2021 watumishi **07**.

vii. Kwa kipindi cha Julai-Septemba 2021 Idara ilipokea watumishi wa Ajira mpya 82 kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kati yao wakiwemo walimu Elimu Msingi 57, Elimu Sekondari 13 na Watumishi wa Afya 12.

viii. **Taarifa ya urejeshwaji wa Watumishi wa darasa la saba kwenye orodha ya Malipo.**

Ilielezwa kuwa Serikali ilitoa maelekekezo kupitia barua ya tarehe 10/07/2017 ya Katibu Mkuu Utumishi ya kuwaondoa watumishi wote ambao walikuwa na Elimu ya Darasa la Saba ambao waliajiriwa baada ya tarehe 20/05/2004 ulipoanza kutumika waraka mpya wa Ajira kwa Watumishi wa Umma na kuhitaji elimu ya Kidato cha NNe kuwa Sifa kuu ya Msingi. Aidha, katika kutekeleza hilo Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze iliwaondoa watumishi 44 wenye elimu ya darasa la saba.

Aidha, serikali ilitoa maelekezo kupitia barua ya Katibu Mkuu ya tarehe 13/04/2018 ya kuwarejesha kwenye orodha ya malipo (kada ya watendaji wa vijiji/Mitaa) watumishi wenye elimu ya darasa la saba ambao waliajiriwa baada ya tarehe 20/05/2004 lakini waliwahi kuajiriwa kwa Mkataba hapo awali. Hivyo, katika kutekeleza agizo hilo Halmashauri iliweza kuwarejesha kwenye orodha ya malipo watumishi 27 watendaji wa vijiji 3 walishafika ukomo kwa kustaafu kabla ya kibali cha kuwarejesha na walipewa kibali cha Kustaafu kazi kwa lazima, watendaji 6 hawakurejeshwa kwasababu kumbukumbu zao zilionyesha kuwa waliwahi kujaza kuwa na Elimu ya kidato cha Nne bila kuwasilisha cheti husika(PRF,OPRAS, BARUA n.k), watendaji 2 hawakurejeshwa walikuwa na vyeti lakini baada ya uhakiki vilikuwa vya kughushi na watumishi wa 6 wakiwemo walimu 2 na watumishi wa Afya 4 hawakurejeshwa kutokana na kutokuwasilisha cheti cha kidato cha nne kama muundo ulivyowahitaji.

Hata hivyo, kutokana na tamko la Serikali la kushughulikia stahiki zao, Watumishi wa Idara za Elimu na Afya ambao bado hawajawasilisha vyeti tayari Ofisi inaendelea na taratibu za kushughulika Stahiki zao.

Aidha, kufuatia Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sherehe za Mei Mosi mwaka 2021, alitoa maagizo ya kushughulikia mafao ya watumishi wa darasa la saba ambao walikuwa hawajaghushi vyeti ambapo maagizo hayo yalitolewa ufafanuzi kupitia barua yenye Kumb. Na. CFC.26/205/01/AM/85 ya tarehe 07/05/2021 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora. Kuhusu kuwaandalia mafao kwa mujibu wa sheria, Kanuni na taratibu watumishi wa darasa la saba ambao hawajaghushi vyeti wala hawakuwahi kujaza taarifa ya kuwa na elimu ya kidato cha nne katika kumbukumbu zao za kiutumishi. Aidha, ilielezwa kuwa Halmashauri ya Chalinze kulikuwa na jumla ya watumishi wa kundi hilo wapatao sita ambapo taratibu za kuwalipa mafao yao zinaendelea.

Watumishi wenye elimu ya darasa la Saba ambao Pia idara ilitekeleza majukumu mbalimbali ya kiutawala ikiwa ni pamoja na:-

ix. Kupokea viongozi mbalimbali waliofanya ziara za kikazi katika Halmashauri ya Wilaya Chalinze
Katika kipindi cha Julai-Septemba 2021 viongozi waliotembelea Halmashauri ni 9 akiwemo na Naibu wa Waziri OR-TAMISEMI, DC-Kisarawe, DC-Bagamoyo, Katibu tawala Mkoa wa Pwani, Mkurugenzi Mtendaji Manispaa Morogoro, Naibu Waziri wa Afya, RC-Pwani, Waziri OR.TAMISEMI.

x. Kuratibu zoezi la vikao vya kisheria vilivyofanyika mwezi Julai-Septemba 2021/2022. Ambapo vikao 17 vilifanyika kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2021

xi. Pamoja na kuratibu na kusimamia vyombo vya Usafiri (Magari ya Halmashauri) Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Chalinze ina vyombo vya usafiri/Magari 22 mazima yanayofanya kazi 13 na mabovu ni 9
Wajumbe walipokea taarifa na kuhoji na kushauri yafuatayo:-

**USHAURI**

Kwenye orodha ya watumishi waliohamia aongezwe Mkaguzi wa ndani Bw. Michael H. Maganga.

**Kuhusu Matumizi ya Magari**

Mjumbe alisema matumizi ya magari ya Ofisi hayapo vizuri na kushauri Suala la matumizi ya gari lizingatiwe, wote wahudumiwe sawa kwenye suala la usafiri.
Ushauri ulipokelewa.

Mjumbe alisema kuna magari mengi mabovu na kushauri magari yote mabovu yatengenezwe kwa wakati. Aidha, kila gari litumike kwa kazi yake kama inawezekana kama inawezekana mfano shughuli za utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

Mwenyekiti alipokea maelezo ya mjumbe na kueleza kuwa ufuatiliaji unaendelea na kushauri fedha zinazodaiwa TEMESA zikalipwe magari yatengenezwe yarudi yaendelee na kazi.

**USHAURI**

i. Mweka Hazina atoe kipaumbele katika suala la matengenezo ya magari
ii. Ratiba ya uhitaji wa gari itolewe mapema

Mwenyekiti alisema ratiba zipo lakini kuna ratiba ambazo hazikwepeki kama za Mtihani na Mwenge.

Kuhusu changamoto ya usafiri Idara ya Ujenzi na kutokana na majukumu yalivyo ilishauriwa gari ya mipango itumike pia na Idara ya Ujenzi kwa kuwa nao pia wanashughulika na miradi ya maendeleo.

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.07/2021-2022 TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI MWEZI JULAI- SEPTEMBA 2021/2022**

Taarifa ya ukaguzi robo ya kwanza 2021/2022 (Julai-Septemba 2021) iliwasilishwa na Idara husika. Taarifa hiyo kwa muhtasari ilieleza kuwa ukaguzi uliofanyika katika kipindi cha robo ya kwanza ilikuwa ni kwa lengo la:-

i. Kuona kama makusanyo yanapelekwa benki kwa wakati.
ii. Kuona kama manunuzi yote yanakatiwa stakabadhi za kielekektronic (EFD receipt)
iii. Kuona kama malipo yanafanyika kwa kuzingatia vifungu vya bajeti
iv. Kuona kama malipo kwa wazabuni yanakatwa kodi za Serikali.

Hata hivyo ilielezwa kuwa kuna kazi ambazo hazikuwa kwenye mpango ambazo zimefanyika katika kipindi hiki ni pamoja na kuhudhuria mafunzo ya mfumo mpya wa taarifa za kiutumishi na mishahara (New HCMIS) yaliyofanyika Dodoma na Mafunzo ya ukaguzi wa Mifumo iliyofanyika Morogoro.

**Utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za mkaguzi wa nje (CAG) kwa mwaka 2019/2020**

Ilielezwa kuwa kwa kipindi kinachoishia Juni 2020, mapendekezo ya Hoja za ukaguzi yaliyotolewa yalikuwa **49**, mapendekezo yaliyotekelezwa na hoja kufungwa yalikuwa **33** sawa na **67%** na mapendekezo yanaendelea kufanyiwa kazi kulingana na maoni ya Mkaguzi. Hoja ambazo hazijafungwa ni **16** sawa na **33%**.

**Utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za mkaguzi wa ndani**

Ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2021 Halmashauri ilikuwa na jumla ya Hoja **8** zenye jumla ya **Tshs 162,718,720.26** ambazo utekelezaji wake unaendelea.

Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya bunge la hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2021 Halmashauri ilikuwa jumla ya maagizo 3 ya kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Kati ya maagizo haya mawili yametekelezwa na agizo moja utekelezaji wake unaendelea. Mchanganuo wa maagizo ni kama ifuatavyo:-

| **NA** | **AGIZO** | **UTEKELEZAJI** |
|---|---|---|
| 1 | Kukamilisha ujenzi wa jengo la mionzi Msoga | Agizo limezingatiwa. Jengo la mionzi katika Hospitali ya Msoga limekamilika. |
| 2 | Kukamilisha kupeleka Tshs 350,000 katika fedha za mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ambazo hazikupelekwa. | Agizo limezingatiwa. Kiasi cha Tshs 350,000 kimepelekwa katika vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu. |
| 3 | Kusitisha mkataba wa ujenzi wa jengo la ofisi za Halmashauri | Agizo limetekelezwa. Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji kwa kutumia "force account" |

Wajumbe walipokea taarifa na kusema kuwa utekelezaji wa agizo moja lililobaki ukikamilika hoja itafungwa. Na hivyo menejimenti inajitahidi kuhakikisha ujenzi unakamilika haraka ili hoja ifungwe na Mkataba usitishwe.

Aidha, ilielezwa kuwa kuna kasoro mbalimbali zilijitokeza wakati wa ukaguzi na baadhi ya dosari hizi zimefanyiwa utekelezaji kama inavyoonekana katika matokeo ya ukaguzi.

i. Mapato yasiyopelekwa benki (defaulters list) **Tshs 20,041,330.06 (Hoja Haijafungwa)**
ii. Malipo yaliyolipwa kwa vifungu visivyo sahihi **Tsh 8,432,469.00(Hoja haijafungwa)**
iii. Malipo yasiyozingatia stakabadhi za kielektroniki (EFD) **Tshs 25,374,753.6 (Hoja imefungwa)**
iv. Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio **Tsh 2,354,022 (Hoja haijafungwa)**
v. Malipo yaliyovuka mwaka wa fedha **Tshs 24,250,000( Hoja haijafungwa)**
vi. Mahamisho ya fedha kwenda akaunti za vijiji bila kuwepo stakabadhi za kukiri mapokezi **Tsh 91,460,960 (Hoja haijafungwa)**
vii. Ukaguzi maalum Kijiji cha Gongo
viii. Ukaguzi maalum Kijiji cha Matipwili
ix. Ukaguzi maalum Kijiji cha Talawanda
x. Ukaguzi maalum wa zahanati ya Kitonga

8. **MATOKEO YA UKAGUZI HUU**

**Hoja Na. 8.1 Mapato yasiyopelekwa benki (defaulters list) Tshs 20,041,330.06**

Ukaguzi ulibaini kuwa hadi tarehe 30 Septemba 2021 mapato ya kiasi tajwa hapo juu yalikuwa hayajawasilishwa benki kutokana na kutokuwepo na ufuatiliaji wa karibu wa mapato ambapo inaweza kusababisha upotevu wa mapato ya Halmashauri.

**USHAURI**

i. Kufanyika kwa ufuatiliaji wa kila siku wa kuhakikisha mapato yote yanayokusanywa yanapelekwa benki kwa wakati
ii. Kuendelea kuchukua hatua kwa kuwasimamisha kazi wahusika ambao hawapeleki makusanyo ya mapato benki.

**Hoja Na. 8.2 Malipo yaliyolipwa kwa vifungu visivyo sahihi (wrong expenditure codes) Tshs 8,432,469.00**

Ilielezwa kuwa ukaguzi uliofanywa kupitia nyaraka za malipo umebaini kuwa malipo yanayofikia Tshs 8,432,469.00 yamefanywa bila kuzingatia vifungu husika vya matumizi hayo. Wajumbe walipokea hoja na kushauri yafuatayo:-

**USHAURI**

i. Kufanya matumizi kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa
ii. Kiasi cha Tshs 8,432,469.00 kirudishwe kwenye kifungu husika ili matumizi yafanyike kama yalivyokuwa yameidhinishwa.

**Hoja Na. 8.3 Malipo yasiyozingatia stakabadhi za kielektroniki (EFD) Tshs 25,374,753.6**

Ilielezwa kuwa ukaguzi uliofanyika katika eneo hili ulibaini kuwa Halmashauri ya Chalinze ililipa **Tshs 25,374,753.6** kwa wauzaji, makandarasi na watoa huduma wengine bila kudai stakabadhi za EFD

USHAURI

Mweka Hazina ajitahidi kufuatilia stakabadhi za kielektroniki (EFD) zipatikane kwa walitoa huduma hoja ifungwe.

Hoja Na. 8.4 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio Tsh 2,354,022

Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Tsh 2,354,022 kililipwa kwa watoa huduma mbalimbali ikiwa ni malipo ya huduma walizotoa kwa Halmashauri bila kukata kodi ya Zuio kwa watoa huduma hao. Aidha, ilielezwa kuwa TRA wanadai fedha za Zabuni tunazotumia ndani ya Halmashauri.

USHAURI

i. Mweka Hazina ajipange akawasiliane na TRA kuona namna ya kufuta deni hilo
ii. Fedha zipelekwe kila mwezi

**Hoja Na. 8.5 Malipo yaliyovuka mwaka wa fedha Tshs 24,250,000**

Ilielezwa kuwa ukaguzi ulibaini kuwepo kwa matumizi mbalimbali yenye jumla ya kiasi cha **Tshs 24,250,000** yaliyostahili kulipwa ndani ya mwaka wa fedha uliopita 2020/2021 badala yake yamelipwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2021/2022. Na hii inasababishwa na kutozingatiwa kwa bajeti ya mpango na matumizi iliyopitishwa na inaweza kupelekea kukwamisha baadhi ya shughuli zilizopangwa kufanyika ndani ya mwaka huu wa fedha.

USHAURI

i. Kuzingatia bajeti na mpango iliyopitishwa na Bunge kwa mwaka husika
ii. Kuandaliwa upya kwa madokezo yaliyovuka mwaka

Hoja Na. 8.6 Mahamisho ya fedha kwenda akaunti za vijiji bila kuwepo stakabadhi za kukiri mapokezi **Tshs 91,460,960**

USHAURI

Wajulishwe watendaji wa vijiji na Kata kukiri mapokezi ya fedha hizi ili hoja ifungwe.

9. UKAGUZI WA VIJIJI

9.1 UKAGUZI WA KIJIJI CHA GONGO

Katika kijiji hicho wakaguzi walikagua upotevu wa kitabu cha kukusanyia mapato na marejesho ya fedha za vikundi vya wanawake na vijana kutokufikishwa Halmashauri ya Chalinze.

**I. Upotevu wa Kitabu cha kukusanyia mapato**

Ukaguzi ulibaini kuwa kitabu kinachodaiwa kupotea na kupatikana bado hakionekani. Aidha, ilielezwa kuwa katika ukaguzi huo kitengo hakikupatiwa uthibitisho wa namba ya kitabu kilichopotea na nakala ya taarifa ya kupotea kwa kitabu husika kwenda polisi.

Aidha, mwenyekiti alihoji kama ushauri wa mkaguzi umezingatiwa

i. Kuhusu kupelekwa Mtendaji Gongo ilielezwa kuwa Mtendaji ameshapelekwa
ii. Kuhusu upotevu wa Kitabu cha makusanyo Mwenyekiti alishauri taarifa ya upotevu wa kitabu ipelekwe polisi. Pia mhusika asimamishwe kazi

iii. Makabidhiano ya Ofisi yafanyike kwa maandishi. Watendaji wakabidhiwe ofisi kwa maandishi

iv. Kutoa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa serikali za vijiji ili waweze kushauri na kutoa elimu kwa wananchi .ilielezwa kuwa mafunzo yatatolewa.

**II. Marejesho ya fedha za vikundi vya wanawake na vijana kutokufikishwa Halmashauri ya Chalinze.**

Ukaguzi ulifanyika kwenye vikundi viwili vya wanawake na vijana ambavyo Ni kikundi cha New Zaraninge Vijana na kikundi cha Zaraninge wananwake na kubaini kuwa fedha ziliwasilishwa Halmashauri na wanakikundi kupatiwa stakabadhi. Aidha, ilielezwa kuwa kikundi cha New Zaraninge GROUP wanawake wanadaiwa Tshs 11,000 na Zeraninge Vijana group Kimange wamekamilisha marejesho.

**USHAURI**

Vikundi vielimishwe namna bora ya kufanya maresho ya mkopo inayotolewa ili kuepukana na uwezekano wa upotevu wa fedha za marejesho.

**9.2 UKAGUZI WA KIJIJI CHA MATIPWILI.**

Ukaguzi uliofanyika Kijiji cha Matipwili ulilenga **kukagua mapato na matumizi ya Kijiji** na **Kuhakiki matumizi mabaya ya fedha za kijiji**

**I.** katika kukagua mapato na matumizi wakaguzi hawakufanikiwa kutokana na kuwa nyaraka zilikuwa TAKUKURU na

**Ii.** Kwa upande wa uhakiki wa Tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za kijiji walibaini yafuatayo:-

- i. Kutokubainika kwa matumizi ya Tshs 3,000,000 zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa pump katika shule ya sekondari matipwili
- ii. Kuchukua na kutumia fedha za Wananchi kupitia Kampuni ya Elvin Agriculture Co.Ltd kiasi cha Tshs 700,000 kila mwaka kuanzia 2016
- iii. Kufuja kwa behewa za chumvi zaidi ya 45 tangu mwezi Juni 2020 hadi Desemba 2020
- iv. Kutumia fedha zitokanazo na ugawaji wa viwanja zaidi ya 200 bila kupelekwa benki na kupata idhini ya matumizi ya Tshs 4,000,000
- v. Kufanya Udanganyifu kwa kutengeneza madawati 54 badala ya madawati 62 yaliyotakiwa kutengenezwa. Kiasi cha Tshs 6,400,000 zilitolewa benki kwa ajili ya kumlipa mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na gharama za fundi kwa kutengeneza madawati 100
- vi. Kutumia fedha za mradi wa uchimbaji wa Rambo la mifugo bila ya kupata ushauri kitaalam kutoka wilayani na kupoteza fedha za wananchi. Tshs 5,160,000/=

**USHAURI**

i. Watendaji wajengewe uwezo

ii. Wananchi wanamtaka mtendaji wa Kijiji aondolewe

iii. Ufanyike utaratibu wa kuandaa kikao na wananchi

iv. TAKUKURU waandikiwe barua ya kuwataka warejeshe nyaraka za kijiji cha Matipwili ili maamuzi yaendelee.

### 9.3 UKAGUZI WA KIJIJI CHA TALAWANDA

Katika kijiji hiki yalikaguliwa mapato, matumizi na Kamati ya usimamizi wa mradi

**(a) Mapato**

Ilielezwa kuwa Kata ya Talawanda ilipokea fedha **Tshs 5,000,000** kutoka katika mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ukarabati wa josho la Mbwewe lililopo katika Kitongoji cha Vundumu.

**(B) Matumizi**

Hadi kufikia tarehe 31/05/2021 kiasi cha **Tshs 4,658,000** kilitumika na kubakia salio la **Tshs 342,000,000 benki**

Kamati ya Usimamizi wa mradi

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa kasoro mbalimbali katika kutekeleza mradi kama ifuatavyo:-

i. Vifaa kununuliwa bila kupokelewa na kuhakikiwa na kamati na kuingizwa kwenye leja ya mali.
ii. Kuwepo kwa vifaa vya ujenzi ambavyo vimeharibika kabisa na vingine vimeanza kuharibika. Tshs 2,280,000
iii. Kuwepo kwa malipo kwa ajili ya vifaa ambavyo havikuonekana wakati wa ukaguzi Tshs 130,000
iv. Kuwepo kwa matumizi ya fedha za miradi bila kuonyesha fedha hizo zimelipwa kwa nani na mchanganuo wa kazi zilizofanyika Tshs 890,000
v. Kuwasilishwa kwa nakala ya mihtasari yote ya kutolea fedha benki
vi. Kamati kushindwa kusimamia mradi ipasavyo jambo lililopelekea mradi kutokutekelezwa kama ilivyopangwa.

Wajumbe walipokea taarifa ya ukaguzi na kushauri yafuatayo:-

**USHAURI**

i. Mihtasari original ya kutoa fedha ibaki ofisi ya Mipango
ii. Ufanyike ufuatiliaji wakina wa suala hili ili lifike mwisho
iii. Mhandisi wa Ujenzi akathibitishe kama vifaa vilipokelewa
iv. Mkaguzi wa ndani akathibitishe kama vifaa vilipokelewa.
v. Mhandisi wa Ujenzi kwenda kuthibitisha kama hiyo mifuko iliyoganda inaweza kufanya kazi
vi. Fedha zirudishwe
vii. Wahusika wachukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kuandikiwa barua za kutoa maelezo juu ya tuhuma zinazowahusu.

### 9.4 UKAGUZI WA ZAHANATI YA KIJIJI CHA KITONGA

Katika kufanya ukaguzi katika Zahanati ya kijiji cha Kitonga yalibainika yafuatayo:-

i. Malalamiko dhidi ya uongozi wa Kijiji (Mwenyekiti) na 1,2,3,6 na 7
ii. Kufanya Matumizi mabaya ya fedha za mradi wa ujenzi wa Zahanati

Ukaguzi wa uendelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Zahanati umebaini yafuatayo:

**MAPATO**

Halmashauri ilitoa fedha kiasi cha Tshs 10,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati katika kijiji cha Kitonga na pia Mhe. Mkuu wa wilaya alitoa Tshs 1,000,000/= kwa ajili ya kutengeneza kivuko cha wanafunzi lakini fedha hizi zilitumika katika ujenzi wa Zahanatihivyo kufanya jumla ya mapato kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati kuwa **Tshs 11,000,000/=**

MATUMIZI

Kulingana na nyaraka zilizowasilishwa fedha kiasi cha **Tshs 11,700,000/=** zilitumika kwa ajili ya uendelezaji wa Zahanati ya Kitonga.

Aidha, ukaguzi ulibaini kasoro zifuatazo:-

i. Kukosekana kwa nyaraka muhimu za kuthibitisha uhalali wa malipo
ii. Utekelezaji wa mradi bila kushirikisha kamati ya Ujenzi
iii. Fedha kiasi cha Tshs 1,000,000/= kutumika kinyume na maelekezo

Wajumbe walipokea taarifa ya ukaguzi wa Ujenzi wa Zahanati ya Kitonga na kushauri yafuatayo:-

**USHAURI**

i. Mkaguzi wa ndani akakague ili kujiridhisha kama fedha Tshs 1,000,000/= zilipokelewa
ii. Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya aende akakague na kutoa ushauri wa Kitaalam.

**HWC/FUM/MUH NA. 03/AG. 08/2021-2022 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA KWANZA 2021/2022**

Taarifa iliwasilishwa na Idara husika. Taarifa hiyo kwa muhtasari ilieleza kuwa Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2021/2022 iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Tshs 21,039,779,950.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30, Septemba, 2021 Jumla ya **Tshs 3,705,978,824.54** kutoka vyanzo vifuatavyo (i) mapato ya ndani ni **Tsh. 1,146,446,483.81** ambayo ni sawa na asilimia **58.2** ya fedha za mapato ya ndani halisi (ii) Ruzuku ya Serikali Kuu ni **Tsh. 544,491,078.93** (iii) Wahisani ni **Tsh. 2,015,041,261.80** na (iv) michango ya jamii ambayo ni kwa upande wa afya na Elimu ilikusanywa **Tsh.570, 577,954.88**. Jumla ya fedha zote zilizopokelewa ni sawa na asilimia 17.03 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Jumla ya kiasi cha **Tsh. 1,392,216,216,628.33** kilitumika sawa na asilimia **37.57** ya fedha zilizopokelewa. Mapato ya ndani jumla ya **Tsh. 949,015,807.27** kilitumika. Serikali kuu na Wahisani zilizotumika ni **Tsh.436, 390,821.16** ambayo ni sawa na asilimia **17.05** ya fedha zilizopokelewa. Fedha nyingi zinazoonekana kutotumika ni za TASAF ambazo taratibu za malipo zilikuwa zinaendelea. Pia Halmashauri ilipokea fedha kutoka Serikali kuu kiasi cha **Tsh. 250,000,000.00** zinazotokana na kodi ya Tozo za simu kwa ajili ya uendelezaji wa kituo cha afya Msata na kiasi cha **Tsh. 47,719,151.8** kwa ajili ya UVIKO-19

Wajumbe walipokea taarifa na kushauri yafuatayo:

**USHAURI**

Afisa mipango na Mweka hazina kufanya usuluhishi wa pamoja ili taarifa zao ziweze kufanana.

**HWC/FUM/MUH NA. 03/AG.09/2021-2022 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI ZA IDARA KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA 2021/2022 (JULAI- SEPTEMBA 2021)**

Taarifa za utekelezaji za Idara robo ya kwanza 2021/2022 (Julai-Septemba 2021) ziliwasilishwa na wajumbe walizipokea taarifa hizo bila kuhoji chochote kwa ajili ya kuzipeleka kwenye Kamati za Kudumu.

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.10/2021-2022 KUPITIA MIHTASARI NA YATOKANAYO YA KAMATI ZA KUDUMU YA ROBO YA NNE APRILI -JUNI MWEZI 2020/2021.**

Mihtasari yote ya kamati za kudumu na yatokanayo yake ya vikao vya robo ya Nne 2020/2021 (Aprili-Juni 2021) na Mwezi iliwasilishwa. Wajumbe walipokea na kujadili kamati moja baada ya nyingine kama ifuatavyo:-

**1. MUHTASARI WA KAMATI YA FEDHA,UONGOZI NA MIPANGO**

Muhtasari na yatokanayo ya kamati ya fedha uongozi na mipango vilipitiwa na wajumbe

Kuhusu akaunti za vitongoji vya mamlaka ya Mji Mdogo Chalinze kuendelea kutumika kwenye vitongoji

***AZIMIO***

***Kuandikwa barua kwenda Benki ya NMB kupata Benki statement ya akaunti za vitongoji vya mamlaka ya Mji Mdogo Chalinze kabla ya kufunga Akaunti hizo.***

USHAURI

Mjumbe alishauri tunapoelekea kufunga akaunti za Mamlaka ya Mji Mdogo Chalinze Halmashauri kujipanga ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa mamala ya mji mdogo Chalinze ipasavyo

**2. MUHTASARI WA KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI.**

Muhtasari na yatokanayo ya kamati ya Elimu, Afya na Maji vilipitiwa na wajumbe.

USHAURI

Kuhusu vibarua wa kujitolea Wakuu wa Idara na Vitengo kusitisha kuleta vibarua hao kwa kuwa bajeti ya kuwalipa haipo.

**3. MUHTASARI WA KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA**

Muhtasari na yatokanayo ya kikao cha Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira vilipitiwa na wajumbe

Kuhusu zoezi la ufanyaji doria ya pamoja kati ya Task Force ya Halmashauri na TFS inafanyika kama ilivyoagizwa na kamati

**HWC/CMT/MUH NA. 03/AG.11/2021-2022 TAARIFA MBALIMBALI**

1. **TAARIFA YA MAPOLEZI YA FEDHA ZA MIPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO -19.**

Mjumbe alieleza kuwa Halmashauri ya Chalinze ni moja kati ya Halmashauri 184 zilizopokea fedha hizo. Halmashauri ya Chalinze imepata mgao wa 1,770,000,000.00 kwa mchanganuo ufuatao

1. Tsh 1,320, 000, 000,00 - Kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 66 vya madarasa kwa Shule za Sekondari,pamoja na viti na meza 3,300.
2. Tsh 280,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 14 kwa Shule Shikizi 5.
3. Tumepata magari mawili kwa ajili ya Idara ya Afya moja ni gari ya Wagonjwa na nyingine ni gari kwa ajili ya usimamizi wa huduma za Afya.
4. Tumepata mgao wa Mashine moja ya mionzi (X-RAY) yenye thamani ya Tsh. 420,000,000.00 kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya Msoga.
5. Tumepokea Tsh.90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mtumishi ya 3 in 1 Hospitali ya Msoga

Wajumbe walipokea taarifa na kushauri yafuatayo;

**USHAURI**

I. Iundwe timu kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi hii. Aidha, ilielezwa kuwa kila darasa likamilike kwa milioni 20 tu pamoja na viti na meza.
II. Usimamizi ufuate Sheria, taratibu na miongozo ushauri ulipokelewa.
III. Wakuu wa Shule na Maafisa Manunuzi wapewe miongozo ya usimamizi wa miradi hii.

Afisa Mipango aliwaeleza wajumbe kuwa miongozo kwenye manunuzi inashauriwa kufanya manunuzi ya pamoja.

1. **TAARIFA YA KUANZISHWA DENTAL CLINIC HOSPITAL YA WILAYA YA MSOGA.**

   Mjumbe ambaye ni Mganga Mkuu alitoa taarifa ya kuanzishwa kwa kliniki ya kinywa na (Meno) Hospitali ya Wilaya ya Msoga kwa kupitia wadhamini ambao wametafutwa na Mh.Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete.

   Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kupongeza jitihada za Mh.Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete katika kuisaidia Chalinze.

**HWC/CMT/MUH NA.03/AG.12/2021-2022 KUFUNGA KIKAO.**

Katibu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti alisema Wakuu wa Idara waende Ofisi ya Utumishi kwa ajili ya kuchukua mikataba pamoja na kuwasilisha taarifa zao zikae kwenye mafaili kama CV, Vyeti vya Taaluma, Vyeti vya ndoa, vyeti vya watoto pamoja na barua za kuthibitishwa kazini na kuthibitishwa Ukuu wa Idara .Baada ya maelezo mafupi alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao ambapo wakati akifunga kikao alisema Watumishi wanachelewa sana kufika kazini na kusisitiza Watumishi kuwahi kazini.Aidha ,aliwashukuru wajumbe kwa Ushirikiano na pia kusisitiza usimamizi makini wa miradi ya fedha zilizotoka IMF kwani zitakuwa na hoja.kwa upande wa stahiki za Wakuu wa Idara alisema pamoja na changamoto zilizopo fedha zilipwe. Pia alisisitiza Watumishi kuchanja chanjo ya COVID-19. Aidha ,alisema uhamishaji ufanyike.

watumishi kujitolea kuhamasisha kuchanja baada ya hapo alifunga kikao saa 10:30 Jioni.

UMETHIBITISHWA NA:-

| | |
|---|---|
| Saini ............................................ | Saini: ............................................ |
| Jina JANE S. MFUKO | Jina: RAMADHANI S. POSSI |
| Cheo DHRO | Cheo: DED |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| TAREHE 19/11/2021 | TAREHE 19/11/2021 |